







# Watoto wa nta

## Les enfants de cire

-  Southern African Folktale
-  Wiehan de Jager
-  Mutugi Kamundi
-  Kiswahili / French
-  Level 2





Hapo zamani za kale, paliishi familia yenye furaha.

...

Il était une fois une famille bien heureuse.

Hawakugombana hata kidogo.  
Watoto waliwasaidia wazazi  
nyumbani na shambani.

...

Ils ne se disputaient jamais. Ils  
aidaient leurs parents à la maison  
et dans les champs.





Lakini, walikatazwa kwenda karibu na moto.

...


Mais ils n'avaient pas le droit de s'approcher d'un feu.



Walifanya kazi zao zote usiku. Hii ni  
kwa sababu walikuwa  
wameumbwa kwa nta.

...

Ils devaient faire tout leur travail  
pendant la nuit. Puisqu'ils étaient  
faits de cire !



Lakini, kijana mmoja alitamani  
kwenda nje wakati wa mchana.

...

Mais un des garçons désirait se  
promener au soleil.



Siku moja tamaa ya kwenda nje ikazidi. Wenzake wakamwonya asiende juani. Lakini, hakusikia.

...

Un jour son désire était trop puissant. Ses frères l'avertirent...

Aliyeyuka kwa sababu joto lilikuwa kali.

...

Mais c'était trop tard ! Il fonda au soleil brûlant.







Watoto wa nta walihuzunika  
walipoona kaka yao akiyeyuka.

...

Les enfants de cire étaient si tristes  
de voir leur frère fondre.



Wakapanga jambo fulani.  
Walichukua nta iliyoyeyuka  
wakatengeza ndege.

...

Mais ils firent un plan. Ils  
façonnèrent le morceau de cire  
fondue en oiseau.



Wakamweka ndege huyo juu ya  
mlima mrefu.

...

Ils apportèrent leur frère l'oiseau  
jusqu'au sommet d'une montagne  
haute.



Jua lilipochozoza asubuhi,  
akapeperuka akiimba kwa furaha.

...

Et lorsque le soleil se leva, il  
s'envola vers la lumière du matin  
en chantant.



# Storybooks Canada

[storybookscanada.ca](http://storybookscanada.ca)

**Watoto wa nta**

**Les enfants de cire**

Written by: Southern African Folktale

Illustrated by: Wiehan de Jager

Translated by: (sw) Mutugi Kamundi, (fr) Alexandra Danahy

This story originates from the African Storybook ([africanstorybook.org](http://africanstorybook.org)) and is brought to you by [Storybooks Canada](http://Storybooks Canada) in an effort to provide children's stories in Canada's many languages.



This work is licensed under a Creative Commons  
[Attribution 3.0 International License](http://creativecommons.org/licenses/by/3.0/).